TANGAZO LA SERIKALI NA 742 la tarehe 30/11/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA. 290)

_____

SHERIANDOGO

_____

Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1)

SHERIANDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanzakutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogoza (Ada naUshuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze za mwaka, 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.

Tafsiri

3. Katika SheriaNdogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

*"Ad*a" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri

*"Afisa Masuuli"*maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze

*"Afisa Mwidhiniwa"*maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Bidhaa "*maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze;

"Kibali' maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli au kazi Fulani;

"kibali cha ujenzi"maana yake ni idhini ya kwanza ya ujenzi inayotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia kanuni za ujenzi mjini;

*"Leseni"*maana yake nikibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, kampuni au taasisi kinachoruhusu kufanyabiashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri;

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanikia ngozi;

"Madini ya ujenzi" maana yake ni kokoto,mawe,changarawe, mchanga, chokaa,marumaru,kifusi,udongo mfinyanzi au chochote kinachochinbwa katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

*"Masoko"*maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaaa au huduma kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

*"Mkataba"*maana yake ni makubaliano yenye nguvu ya kisheria ya ununuzi au uuzaji au utoaji wa hudumayoyote kati ya Halmashauri na mdauhusika.

*"Mkurugenzi"*maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya

Mkurugenzi;

"Ushuru*"*maanayake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala kwa ajili ya huduma, mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

*"Ushuru wa Madini ya Ujenzi"*maanayake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala na wanunuzi au wasafirishaji wa madini ya ujenzi;

*"Wakala"*maana yake ni mtu, taasisi,kampuni au asasi yoyote iliyeteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri;

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada naUshuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye Jedwali la Kwanzala Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla kifungu 4(1) cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika vyanzo vifuatavyo:-

i. Ushuru wa Mazao
ii. Ada za leseni
iii. Ada za vileo
iv. Ada ya kununu azabuni za Halmashauri
v. Ushuru wa samaki.
vi. Ushuru wa madini ya ujenzi.
vii. Ada ya kukodisha mali za Halmashauri;
viii. Ushuru wa Machinjio, Ukaguzi wa nyama na Ada ya Bucha;
ix. Adana ushuru wa kuendesha shughuli za Utamaduni, burudani na michezo;
x. Ada ya Upimaji wa ardhi na vibali vya ujenzi;

xi. Ushuru wa soko
xii. Ada ya zabuni

Namna ya kukusanya Ada naUshuru

5 (1) Halmashauri itaweka utaratibu itakavyoona inafaa ikiwani pamoja na kutenga maeneo maalum ya kutoza Ada na Ushuru kutoka vyanzo vya mapato kama ilivyo ainishwa kwenye kifungu 4(2) cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Malipo ya Ada au Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(3) Ada na Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa wakati au kabla ya kupata huduma husika.

(4) Bilakuathirimasharti ya kifungu 5(2) cha Sheria Ndogohizi Halmashauri au wakala kwa idhini ya Afisa Masuuli itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika endapo stakabadhi ya kielektroniki haiwezi kutolewa.

(5) Halmashauri au wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au wakala haitalipiwa Ushuru unaodaiwa ndani ya siku 7 kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na ndani ya siku 2 kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka. Halmashauri itaomba idhini ya Mahakama ili kuuza bidhaa au mali na fedha zitakazopatikana zitawekwa kwenye akaunti ya Halmashauri

(7) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanyajambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.

Wajibu wa kulipaAda auUshuru

6 (1) Ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kulipa kiwango cha Ada au Ushuru kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

7. (1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mfanyabiashara au mtu yeyote anayetaka kufanya jambo lolote linalohitajiki bali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

Uteuzi wa wakala

8. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteuaKampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini yakifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:

(a) Kukusanya na kupokeaUshuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alililopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Kukusanya Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilishamakusanyo yote kwa kuzingatiamasharti ya mkataba wa uwakalaalioingia na Halmashauri.

Makosa kwa Wakala

10. Itakuwani kosa kwa Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-

(1) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ushuru.

(3) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogohizi.

(4) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ushuru ndani ya Halmashauri

(5) atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ushuru.

(6) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ushuru.

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa nia ya kukusanya au kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusiana na Ada, Ushuru, leseni au Kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

12. Itakuwani kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

1) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataakulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
2) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ushuru.

3) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
4) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri.
5) atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.
6) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Kufifilisha Makosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000/=) mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatanishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa fedha anazodaiwa.

Adhabu

14. Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tsh .200, 000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (Tsh. 1,000,000/=)au kifungo kisicho pungua miezi kumi na mbili na kisicho zidi miezi ishirini na nne.

JEDWALI LA KWANZA
Limetungwa chini ya kifungu cha 4(1)cha Sheria Ndogo hizi

SEHEMU YA KWANZA

SEHEMU B

Ushuru wa Mazao ya kilimo

Na.	*Aina ya mazao*	*Kiwango*
1.	Miwa	3% ya Bei ya kununulia
2.	Pamba	3% ya Bei ya kununulia
3.	Kahawa	3% ya Bei ya kununulia

4.	Maharage	3% ya Bei ya kununulia
5.	Mpunga	3% ya Bei ya kununulia
6.	Mahindi	3% ya Bei ya kununulia
7.	Alizeti	3% ya Bei ya kununulia
8.	Korosho	3% ya Bei ya kununulia
9.	Vitunguu	2% ya Bei ya kununulia
10.	Nazi	2% ya Bei ya kununulia
11.	Viazi mviringo	2% ya Bei ya kununulia
12.	Magimbi	2% ya Bei ya kununulia
13.	Ndizi	2% ya Bei ya kununulia
14.	Nyanya	2% ya Bei ya kununulia
15.	Mihogo	2% ya Bei ya kununulia
16	Mananasi,maembe na matunda yote yalimwayo ndani ya Wilaya	2% ya Bei ya kununulia
17	Bamia na nyanyachungu	2% ya Bei ya kununulia
18	Mboga mboga	2% ya Bei ya kununulia
19	Ufuta	3% ya Bei ya kununulia

SEHEMU YA PILI
SEHEMU B

Ada ya kukodi mali za Halmashauri

Na.	*Huduma*	Kiwango
1.	Kukodi Ukumbi wa Halmashauri	100,000/ kwa siku
2.	Viti vya Halmashauri	300/= kwa kila kiti kwa siku
3.	Meza za Halmashauri	400/= kwa kila meza kwa siku

SEHEMU C

(*Ushuru wa Huduma za Machinjio*)

Na.	*Aina ya Mifugo*	*Kiwango*

1.	Ng'ombe	2,000/= kila mmoja
2.	Mbuzi	1,000/= kila mmoja
3.	Kondoo	1,000/= kila mmoja
4	Nguruwe	1500/= kila mmoja
5.	Ada ya ukaguzi na usajili wa gari la kubebea nyama	15,000/= kila mmoja kwa mwaka
6.	Ada ya kusajili mchunaji wa nyama	10,000/= kila mmoja kwa mwaka
7.	Ushuru wa maziwa 5% ya bei ya kununulia	Kwa lita
8.	Ushuru wa ngozi ya ng'ombe tsh 100 kwa asilimia, mbuzi na kondoo TSH 50 kwa kipande	Kwa asilimia 5% kwa kila kipande
9	Pembe za ng,ombe 5% ya bei ya kununulia	Kwa bei ya kununulia
10	Kusafirisha mayai ya kutotolesha tsh 200 kwa kila tray (yakienyeji na yakizungu)	Kwa tray
11	Ushuru wa kusafirisha vifaranga kuanzia 700 ni Tsh 2000 na vifaranga chini ya 700 wasiopungua 300 ni Tsh 1000	Kwa tray
12	Ushuru wa kusafirisha kuku ni Tsh 200 kwa kuku mmoja	Kwa bei kununulia

SEHEMU D

(Ushuru huduma wa Ukaguzi wa Nyama)

Na.	*Aina ya Mifugo*	*Kiwango*
1.	Ng'ombe	2,000/= kila mmoja
2.	Mbuzi	1,000/= kila mmoja
3.	Kondoo	1,000/= kila mmoja

SEHEMU E

(Ada ya ukaguzi na upimaji wa afya kwa wahudumu)

Na.	AINA	KIWANGO Tsh
1	Nyumba za starehe,vilabu vya pombe za kienyeji na nyumba ya kulala wageni,bar na migahawa	5,000/= kila baada ya miezi sita kwa kila mhudumu
2	Maduka ya bidhaa na mama lishe na baba lishe na wauza vyakula vya aina yoyote kwa matumizi ya binadamu	2,000/= kila baada ya miezi sita kila mhudumu
3	Nyumba za kutengeneza na kuuziwa vyakula na nyama choma	3 ,000/= kila baada ya miezi sita kwa kila mhudumu
4	Ukaguzi kwa maombi ya kufungua biashara	10,000/=
5	Ukaguzi kwa maombi ya kufungwa biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya	10,000/=
6	Ukaguzi wa viwanda vikubwa	200,000/= kwa mwaka
7	Ukaguzi wa viwanda vya kati	100,000/=Kwa mwaka
8	Ukaguzi wa viwanda vidogo	50,000/= kwa mwaka
9	Ukaguzi wa wahudumu wa vyakula katika bar hoteli	15,000/= kila baada ya miezi sita

SEHEMU F

(Ushuru wa shughuli za Utamaduni na Sanaa)

ADA YA KIBALI CHA BURUDANI

Na.	*Maelezo*	*Kiwango*
1.	Waganga wa tiba za asili	50,000/=kwa mwaka
2.	Taasisi	100,000/=kwa mwaka

3.	Wauzaji wa dawa za asili/kienyeji	20,000/=kwa mwaka
4	Kibali cha kupigisha dansi na muziki	30,000/=kwa tukio 15,000/= kwa tukio

SEHEMU J

(Ada na ushuru wa Ardhi)

Na.	*Shughuli*	*Kiasi*
1.	Maombi ya mabadiliko ya Makazi kuwa biashara	20,000/=
2.	Maombi ya mabadiliko ya Biashara kuwa Viwanda	20,000/=
3.	Maombi ya mabadiliko ya Makazi kuwa biashara	20,000/=
4.	Maombi kugawanya Kiwanja au Shamba	25,000/=
5.	Maombi ya kuhakiki Umiliki	25,000/=
6	Kibali cha mauziano ya ardhi na Viwanja	Tshs 10,000/= kwa kila mauziano ya ardhi yenye thamani chini ya Tshs million 100 na Tsh 40,000/= kila mauziano ya ardhi yenye thamani zaidi ya million zaidi ya million 100
7	Ushuru wa mauziano ya ardhi	Mauziano baina ya serikali na mtu binafsi au kampuni au baina ya mtu binafsi na mtu binafsi mgawanyo utakuwa kama ifuatavyo; • Halmashauri ya wilaya itapata 10% ya thamani ya mauzo ya ardhi • Kata husika itapata 10% ya kiasi ilichopata Halmashauri ya Wilaya • Kitongoji husika 10% ya kiasi ilichopata Halmashauri ya Wilaya Na mauziano hayo yatashuhudiwa na

		kusimamiwa na mamlaka zinazotambulika kisheria katika Halmashauri

SEHEMU H

(Ushuru wa Maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi)

Na.	*Shughuli*	*Kiasi*
1.	Maombi ya mabadiliko ya Makazi kuwa biashara	20,000/=
2.	Maombi ya mabadiliko ya Biashara kuwa Viwanda	20,000/=
3.	Maombi ya mabadiliko ya Makazi kuwa biashara	20,000/=
4.	Maombi kugawanya Kiwanja au Shamba	25,000/=
5.	Maombi ya kuhakiki umiliki	25,000/=
6	Kibali cha mauziano ya ardhi na Viwanja	Tshs 10,000/= kwa kila mauziano ya ardhi yenye thamani chini ya Tshs million 100 na Tsh 40,000/= kila mauziano ya ardhi yenye thamani zaidi ya million 100.
7	Ushuru wa mauziano ya ardhi	Mauziano baina ya serikali na mtu binafsi au kampuni au baina ya mtu binafsi na mtu binafsi mgawanyo utakuwa kama ifuatavyo; • Halmashauri ya Wilaya itapata 10% ya thamani ya mauzo ya ardhi • Kata husika itapata 10% ya kiasi ilichopata Halmashauri ya Wilaya • Kitongoji husika 10% ya kiasi ilichopata Halmashauri ya Wilaya Na mauziano hayo yatashuhudiwa na

		kusimamiwa na mamlaka zinazotambulika kisheria katika Halmashauri

SEHEMU I

(Ushuru wa Minada ya Mifugo)

Na.	*Aina ya Mnyama*	*Kiwango*
1.	Ng'ombe	3,000/= kwa kila aliyenunua
2.	Mbuzi	2,000/= kwa kila aliyenunua
3.	Kondoo	2,000/= kwa kila aliyenunua

SEHEMU L

(Ada ya unyonyaji maji machafu)

Na.	*Eneo*	*Kiasi*
1.	Eneo la Biashara	80,000/= kwa tripu moja
2.	Eneo la Makazi	60,000/= kwa tripu moja
3 .	Eneo la viwanda	100,000/= kwa trip moja

SEHEMU M

(Ushuru wa kuogesha mifugo)

Na.	*Aina ya Mifugo*	*Kiwango*
1.	Ng'ombe/ ndama	200/= Kila mmoja/ 100 kwa kila mmoja
2.	Mbuzi	100/= kila mmoja
3.	Kondoo	100/= kila mmoja
4.	Farasi	200/= kila mmoja
5.	Punda	200/= kila mmoja

SEHEMU O

Ushuru wa Masoko, Magulio na Minada)

Na.	*Aina ya shughuli*	*Kiwango*
1.	Kuuza nguo za mitumba kwenye gulio au mnada	1,000/=
2.	Kuuza nguo mpya kwenye gulio au mnada	1,000/=
3.	Kuuza Nyama kwenye gulio au mnada	5,000/=
4.	Bidhaa za Urembo kwenye gulio au mnada	1,000/=
5.	Vyombo vya ndani kwenye gulio au mnada	1,000/=
6.	Meza ya kuuzia bidhaa sokoni	200/=
7.	Banda la kuuzia kuku sokoni, gulioni au Mnadani	200/=
8.	Uuzaji wa pumba	Kwa bede 100/=

SEHEMU P

(Ushuru wa Minara)

Na.	*Aina ya shughuli*	*Kiwango*
1.	Kibali cha kuweka mnara wa simu kwa kila mnara	500,000/=

SEHEMU Q.

(Ada ya uzoaji taka ngumu)

Na.	*Maelezo*	*Kiwango*		
		Siku	Wiki	Mwezi
1.	Bar & Hotel na vilabu vya pombe ya kienyeji		2,500/=	10,000/=
2.	Mashine ya kusaga na kukoboa nafaka		1,000/=	4,000/=
3.	Saluni za kike na kiume		1,000/=	4,000/=
4.	Viwanda vidogovidogo(seremala, mafundi sofa na fundi cherehani)		2,500/=	10,000/=
5.	Gereji(pikipiki na magari)		2,500/=	10,000/=
6.	Waosha magari na pikipiki		2,000/=	8,000/=
7.	Migahawa/ mama na baba lishe, chips		1,500/=	6,000/=

8.	Wauza samaki na kuku wa kukaanga		1,000/=	4,000/=
9.	Maduka ya jumla na rejareja		2,000/=	8,000/=
10.	Mabucha ya nyama na samaki		2,000/=	8,000/=
11.	Wafanya biashara ndogondogo (matunda, karanga, wachoma mahindi na magenge)	200/=		
12.	Magari yanayoshusha mizigo(malipo ni kwa mmiliki wa mzigo)	5,000/=		
13.	Maegesho ya Teksi na pikipiki	200/=		
14.	Nyumba za kulala wageni		2,000/=	8,000/=
15.	Nyumba za kuishi		500/=	2,000/=
16.	Taasisi		5,000/=	20,000/=
17.	Zahanati binafsi		2,500/=	10,000/=
18.	Vituo vya mafuta		3,500/=	14,000/=

SEHEMU R

ADA /USHURU MWINGINE

No.	AINA	KIWANGO
1	Ushuru wa bima /kamisheni	2.5% ya bei ya makusanyo
2	Ushuru wa chumvi	500/= kwa kila kg 50
3	Ushuru wa mnada wa jumla wa kitu kinachonadiwa	5% ya bei ya mnada
4	Choo cha umma cha kulipia	200/=
5	Kibali cha kufyatua matofali	30,000/= kwa miezi sita
6	Ushuru wa nyumba za kulala wageni (hotel levy)	10% ya bei ya kitanda kwa siku
7	Ada ya zabuni	50,000/= kwa kila mmoja

JEDWALI LA PILI
KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa (Chini ya kifungu cha 13)cha Sheria Ndogo hizi

Mimi ……wa S.L.P…….…….. nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya…….ambayeni Mkurugenzi Mtendaji

wa Halmashauri ya Chalinze kwamba mnamo tarehe……ya Mwezi….Mwaka……nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo za (Ada naUshuru) za Halmashauri Wilaya ya Chalinze za mwaka 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri .Niko tayari kulipa kiasi cha Ada na Ushuru ninayo daiwa pamoja na faini.
NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIYARI YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……..ya mwezi……mwaka……

Jina……..……...Saini…….....

Mbele ya:

Jina……..…….

Saini…….....

Wadhifa……

Nembo ya Halmashauri ya wilaya ya chalinze imebandikwa kwenye SheriaNdogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe ..... mbele ya:-

EDES PHILIP LUKOA
Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze

L.S

SAIDI OMARI ZIKATIMU
Mwenyekiti Halmashauri ya Chalinze

Dodoma,
4 Octoba, 2018

NAKUBALISELEMANI S.JAFO (MB.)
Waziri Wa Nchi- Or - Tamisemi